بسم الله الرّحمن الرحيم

25/Safar/1427H=25/March/2006Ad,Madinatul Rassuuli llahi {s.a.w} - Saudi Arabia.makala namba 3.

# HII NDIYO DAAWA YETU

## JUU YA UFAHAMU WA SALAF SWALIHI

ATHARI MBAYA YA UZUSHI KATIKA UISLAMU.

قال شيخ الإسلام ابن تيمية:
وأما اتخاذ موسم غير المواسم الشرعية كبعض ليالي شهر ربيع الأول يقال أنها ليلة المولد من البدع لم يستحسنها
السلف ولم يفعلوها"؟

Amesema Sheikhul Islami Ibn Taymiyyah;
[Ama kuufanya msimu isiyokuwa misimu ya kisheria,kama vile baadhi ya nyusiku za mwezi wa mfunguo sita ambazo huitwa usiku wa maulidi ni katika BID'A ambazo hawakuziona nzuri waliotangulia wala hawakuzifanya].

MUANDISHI;

ABUL FADH'LI QASSIM MAFUTA QASSIM.

بسم الله الرّحمن الرحيم

## UTANGULIZI

Sifa zote njema,ni stahiki ya Allah{s.w.t} Bwana wa viumbe wote,na swala na salamu zimfikie Mtume wetu Muhammad {s.a.w} Mbora waviumbe wote,na pia ziwafikie Jamaa zake,na Maswahaba zake wote,na walio waandamia hao kwa wema,mpaka siku ya malipo.

Ama baada ya utangulizi.

Ndugu msomaji! Ukiwa unafuatilia mfululizo wa makala zetu;
HII NDIYO DAAWA YETU.
Hii ni makala namba tatu ambayo inaendeleza mfululizo wa jawabu juu ya hoja dhaifu za watetezi wa bid'a na hii hapa ni;

**Hoja yao ya nne;**

Kama maulidi hayafai mbona sheikh wenu Sheikhul Islami ibin Taymiyyah anayakubali Maulidi,na kuyatetea mpaka kufikia kusema;

**فتعظيم المولد واتخاذه موسما,
قد يفعله بعض الناس ويكون له فيه أجر عظيم لحسن قصده وتعظيمه لرسول الله صلى الله عليه وسلم.**

[Kuyaadhimisha maulidi(ya mtume(s.a.w.),na kuyafanya ni msimu,wanayafanya baadhi ya watu,na watapata ndani yake ujira mkubwa,kwa uzuri wa makusudio,na kumuadhimisha Mtume{s.a.w.}.
tazama Iq'tidhaus siratil mustaqim juzuu 2,ukurasa 126.

**Jawabu yetu ni kama ifuatavyo;**

1-kama utayachukua maneno haya kama yalivyo bila ya kuangalia mnasaba wa wake,kweli utasema Sheikhul Islami anayakubali maulidi na kuyatetea.

Lakini ukizingatia mnasaba wa yeye kuzungumza maneno haya,kwa kufuatilia tangu alipoanzia mpaka kufikia hapo,utagundua kwamba mwanawachuoni huyo yuko mbali kabisa na fikra za wazushi.

Hebu tukudondolee kidogo halafu wewe mwenyewe ndugu msomaji utapata jawabu ya kukukinaisha,hivi kweli mtu anaye yakubali maulidi seuze kuyatetea anasema hivi;

"وأما اتخاذ موسم غير المواسم الشرعية كبعض ليالي شهر ربيع الأول يقال أنها ليلة المولد,من البدع لم يستحسنها السلف ولم يفعلوها"؟

[Ama kuufanya msimu isiyokuwa misimu ya kisheria,kama vile baadhi ya nyusiku za mwezi wa mfunguo sita,ambazo huitwa usiku wa maulidi ni katika BIDAA ambazo hawakuziona nzuri waliotangulia wala hawakuzifanya]?

Hivi kweli anaye yakubali maulidi husema hivi;-

,وكذلك ما يحدثه بعض الناس اما مضاهاة للنصارى فى ميلاد عيسى عليه السلام"
واما محبة للنبي صلى الله عليه وسلم
من اتخاذ مولد النبي صلى الله عليه وسلم عيدا, وتعظيما له والله قد يثيبهم على هذه المحبة والاجتهاد لا على البدع

ولو كان خيرامحضا أوراجحا لكان السلف رضي الله عنهم أحق به منا , اختلاف الناس فى مولده فانهم أشد محبة لرسول الله صلى الله عليه وسلم وهم على الخير أحرص منا.

[Na vilevile yale waliyo yazusha baadhi ya watu,ima ni kujifananiza na wakristo katika(kuadhimisha) mazazi ya Issa(a.s.) na ima ni kwa ajili yakumpenda mtume{s.a.w.} na kumuadhimisha yeye,mwenyezi mungu huwenda akawapa thawaba kwa mapenzi yao haya, na ij'tihadi,na si kwa uzushi wa kuyafanya maulidi ya mtume{s.a.w.}kuwa ni eid.

Basi LAU INGEKUWA NI KHERI tupu,au kheri yenye nguvu,basi waliotangulia-maswahaba-wangekuwa wana haki zaidi (ya kufanya hilo)kuliko sisi ,kwasababu wao wanampenda mtume zaidi kuliko sisi, na wao wanaipupia kheri zaidi kuliko sisi…".

tazama maneno hayo katika kitabu chake Iqtidhaus siratwil mustaqim juzuu 2, ukurasa 123.

Kwa ufupi ni kwamba,sheikhul Islami anaona kwamba;

-kuweka misimu ya sherehe katika dini,kama msimu wa maulidi katika mwezi wa mfunguo sita ni kuzusha katika dini,
swali, je anae yakubali maulidi na kuyatetea husema hivyo?

-Kukusanyika kwa ajili ya maulidi ni bidaa,kwasababu waliotangulia hawakulifanya hilo,
swali, je anae yakubali maulidi na kuyatetea husema hivyo?!

-Mambo haya ya maulidi hayana kheri yoyote,na lau kama mambo haya yana kheri,basi wangeyafanya watu waliotangulia-maswahaba wa mtume{s.a.w.}-

Je mtetezi wa maulidi husema hivyo?!

Huwenda mwenyezi mungu akawapa thawabu baadhi ya watu kwasababu ya ij'thadi yao, yaani wamejitahidi-na hali wao wamefikia daraja hiyo ya ij'tihadi- kwa kudhani kwamba jambo hili ni katika mambo ya kheri, kumbe si kheri.

Bali ni katika mambo ya uzushi,huwenda mwenyezi

mungu akawapa thawabu,kwa ij’tihadi yao hiyo,na si kwasababu ya uzushi. Je na nyinyi ni ulamaa muj'tahiduun?!

Semeni ndiyo ulimwengu wa wasomi uwacheke,ama kwa wasio jua hatamkisema nyinyi ni maswahaba watasema ndiyo!

-Kwasababu mwanawachuoni ambaye amefikia daraja ya ij’tihadi atakapojitahidi -katika mas’ala ambayo yanafaa ij’tihadi ndani yake- kisha akapatia atapata ujira mara mbili, ujira wa kupatia,na ujira wa kujitahidi,na atakapo jitahidi kisha akakosea,atapata ujira mara moja ujira wa kujitahidi tu,na mas’ala haya yameelezwa kwa kina na maulamaa wa usuul kwenye vitabu vya elimu ya usulul fiq’hi.

Na suala hili ndilo analo lizungumzia Sheikhul Islami ibin Taymiyya tangu huko mwanzo mpaka kufikia hapo,na kutoa mifano ya wanawachuoni -muj’tahiduna-wanavyo kosea katika mas’ala mbaliambali,pamoja na hivyo wanastahiki kupata ujira kwasababu ya ij’tihadi yao,.

Na ukitaka kulibaini hili hebu anza kusoma mas’ala hayo kwenye kitabu chake hicho kuanzia aliposema;

"فمن ندب الى شيئ يتقرب به الى الله أو أوجبه بقوله أو بفعله فى غير أن يشرعه الله فقد شرع من الدين ما لم يأذن به الله,نعم قد يكون متأولا فى هذا الشرع,فيغفرله لأجل اجتهاده اذا كان مجتهدا الاجتهاد الذي يعفى معه عن المخطئ,ويثاب أيضا على اجتهاده,لكن لايجوز اتباعه فى ذلك ..."

[na yule ambaye atalifanya kuwa ni sunna jambo lolote ambalo anajikurubisha kwa mwenyezi mungu,au akalifanya kuwa ni wajibu,kwa kauli yake au kwa kitendo chake,pasi na kuwa mwenyezi mungu ndiye aliyeliweka,basi atakuwa ameweka katika dini jambo ambalo hakuliidhinisha mwenyezi mungu.

Naam,inawezekana akawa nimwenye kufanya taawili(tafsiri) katika sheria hii,basi atasamehewa kwa ajili ya ij’tihadi yake itakapo kuwa(yeye) ni muj’tahidi ij’tihadi ambayo husamehewa mwenye kukosea,na atapewa

thawabu vilevile kwa ij'tihadi yake,lakini haitofaa kumfuata katika jambo hilo…].
Tazama al Iqtidhau cha Ibin Taymiyya Juzuu 2,ukurasa 84.

Kwahiyo ukiyaanzia hapo maneno ya Sheikh huyu,mpaka ukifikia hapo kwenye maneno ambayo watetezi wa uzushi wanadai kwamba Sheikhul Islami ameyatetea maulidi,utagundua namna ndugu zetu wanavyo babaika,na namna wasivyokuwa na uwezo wa kuyasoma na kuyaelewa maneno ya maulamaa.

Jambo ambalo linapelekea kwenye upotoshaji wa haki.
Na ndiyo pale katika yale maneno ya ibin Taymiyya waliyo yafanya kuwa ni hoja ya kufaa kwa maulidi
utaikuta ibara hii;

...قد يفعله بعض الناس
[wanayafanya baadhi ya watu…] baadhi ya watu wenyewe ni hao wanawachuoni wanaoitwa muj'tahidina,na si mtu yoyote.

2-maneno hayo ya Imamu Ibin Taymiyyah tuliyo yataja hapo nyuma pamoja na hayo maneno ambayo wameyaegemea watetezi wa maulidi,kuwa ndiyo hoja yao ya kufaa kwa maulidi yote hayo ameyataja Ibin Taymiyyah kwenye kitabu chake
Iq'tidhau swiratil mustaqim fii mukhalafati as'habil jahim.

Na bila shaka ndugu zetu hawa walipo kuwa wanayanukulu maneno hayo wanayo yategemea juu ya kufaa kwa uzushi wa maulidi waliyaona hayo maneno mengine ya Imamu Ibin Taymiyyah ambayo yanaya vunja hayo wanayo yategemea, kama ndivyo basi mbona wameyanyamazia kimya?

Au walijua kwamba vitabu vya Ibin Taymiyyah wanavyo peke yao hapa duniani? hata kama watayaficha watu hawawezi kuwafichua?

Sasa hebu tujibuni kwa elimu,na ukweli;

Hivi hayo maneno ya Ibin Taymiyyah hamkuyaona? Vipi msiyaone haya mkayaona hayo? na kama kweli hamkuyaona basi sisi tumesha waonyesha namba ya juzuu na sahifa, je mnasemaje?

Au bado mna ng'ang'ania tu kwamba Ibin Taymiyyah anayakubali maulidi na kuyatetea mkaendelea kusherehekea kwa kupiga ngoma na huku mkiimba na kucheza?

Inatakikana mfahamu kwamba, Sheikhul Islami Ibin Taymiyyah ni miongoni mwa maulamaa mabingwa wa fani jadal na usulul fiq'hi tena aliye bobea katika fani hizo kwahiyo unapo soma vitabu vyake wacha pupa na kupapatika,tuliza akili yako na uwe makini huku ukiwa umebeba hazina kubwa ya elimu ya dini,hapo ndiyo utamuelewa bingwa huyo na kufaidika na hazina ya elimu yake,kinyume cha hivyo utakumbwa na mpapatiko huu ulio wakumba ndugu zetu watetezi wa uzushi wa maulidi kwasababu ya kudhani kwamba kila kishindo ni kwa ajili yao.

3-Hata kama ni kweli Sheikhul Islami ibin Taymiyyah amesema maneno hayo kuutetea huo uzushi wa maulidi,bado maneno yake siyo hoja wala dalili ya kisheria, kwasababu yeye si hoja katika dini,bali anaposema au kutenda jambo lolote lile hutakiwa hoja ya kisheria juu ya jambo hilo.

Na bila shaka kwenye jambo hilo wanakubaliana watu wote,wapenzi wa Ibin Taymiyyah,na maadui zake ambao ndio hao walioyatumia maneno yake hayo kimakosa ili wawanyamazishe wapenzi wake,
kwa kuwaambia;

Nini nyinyi,mnapinga maulidi!!mbona sheikh wenu mwenyewe ameyakubali,hebu fungueni sahifa kadha wa kadha….!! bila ya haya wala kuona vibaya kumzulia mwanawachuoni mkubwa kama huyu!!

Bila shaka ndugu msomaji mpaka hapo umeugundua ubabaishaji wa ndugu zetu watetezi wa bidaa,na namna wasivyo kuwa na hoja za kutetea bidaa zao potofu,na namna wanavyo papatika pindi wanapotakiwa kusimamisha hoja za kisheria,na namna walivyo majasiri katika kuipindisha sheria ya Allah {s.w.t.} ili watimize malengo yao na az'ma zao mbaya !!!

na kwahilo wako tayari kuwazulia watu bila kujali wala kuogopa- Sub'haana llah- ni Ujasiri mkubwa ulioje huo?!!

**Hoja yao ya tano;**

Ni hoja ya kiakili,wanasema kwamba;

Hata kama mikusanyiko kama hii ya maulidi haikuweko katika zama Za mtume {s.a.w.} haifahamishi kwamba kufanya ni bidaa,au ni haramu,kwasababu jambo hili linaingia katika mlango wa kuacha,na kuacha siyo dalili,bali ni kukosekana dalili,na kukosekana dalili siyo dalili.

**Jawabu yetu ni kama ifuatavyo;**

Hii ni moja ya miongoni mwa hoja zao ambazo ni nyonge kabisa zisizo na uzito wowote,kama ndugu yangu muislamu utazizingatia hoja tulizo tangulia kuzitaja huko nyuma basi unaweza kuijibu hoja hii kwa urahisi,hasa ukizingatia kwamba hoja yenyewe ni ya kiakili na si yakisheria,
na kwa bahati nzuri na wewe unaakili yako,kwahiyo kila mwenye akili timamu ya kufikiria kwa kina anaweza kuijibu hoja hii,na wala haihitajii elimu kubwa,kwasababu unaweza kuijibu kwa kuhoji tu,kama ikiwa kuwacha siyo dalili,bali ni kukosekana dalili.

Basi ni vipi kuhusu adhana katika swala ya eid?nayo pia inaingia katika mlango huu,yaani ni katika vitu vilivyoachwa na Mtume{s.a.w.} na kuacha kwake siyo dalili ya kwamba kufanya ni bidaa?

Mbona Ibin mas'oud{r.a.}anawakataza watu jambo kwa hoja ya kwamba jambo hilo halikufanywa na mtume{s.a.w.}?!

## Hoja yao ya sita;

Mawahabi ni watu waovu sana,wanawakataza watu wasikusanyike kwa ajili ya kumswalia Mtume{s.a.w.}na kuadhimisha mazazi yake,lakini wao kila mwaka kule Saudia wana wiki nzima(Us'buu Shaikh) ya kumsherehekea Sheikh wao Muhammad bin Abdil wahabi! Sasa ndugu waislamu ninani aliye nahaki ya kusherehekewa?! Muhammad bin Abdil wahabi,au Mtume{s.a.w.}??

Hii si hoja ya kielimu,ni hoja ya kimtaani,lakini kwasababu masheikhe wao pia wanaitumia ndiyo maana tunaijibu.

## Jawabu yetu ni kwa njia tatu;

1-Kwanza kabisa maneno hayo ni ya urongo,na mwenyezi mungu anasema katika Qur'an;

**قتل الخراصون.**

[wamelaaniwa warongo] sura ya 51 aya ya 10,tazama tafsiri ya aya hiyo kwenye Jalaalayn.

Labda tuelezee kwa ufupi ukweli ukoje;

Mnamo siku ya juma mosi,tarehe 08/3/1980 hadi siku ya al hamisi tarehe 14/3/1980,uongozi wa chuo kikuu cha kiislamu,Muhammad bin soud kilichopo Riyadh mji mkuu wa Saudi Arabia,uliandaa semina maalumu katika ukumbi wa mikutano wa king Faisal chuoni hapo,

Semina hiyo ilihudhuriwa na maulamaa wakubwa wa kiislamu kutoka sehemu mbalimbali za dunia,

miongoni mwa maulamaa hao ni;

1-Sheikh  Muhammad bin Ibrahim,mufti wa Saudia wakati huo.

2-Sheikh Abdul Aziz ibin Baaz,Raisi wa chuo kikuu cha Madina wakati huo.

3-Sheikh Wah'bat Azzuhaily muandishi maarufu kutoka Syria.

4-Sheikh Atwiyya bin Saalim,muhadhiri katika msikiti mtukufu wa Mtume{s.a.w.}.

5-Sheikh Mannau bin Khalil al Qattwan,mwandishi wa kitabu Mabahithu fi ulumil Qur'an,kutoka Kuwait.

na wengineo wengi ambao ilifika idadi yao maulamaa 150.

Lengo kuu,na madhumuni ya semina hiyo ni kuwataka wataalamu hao kuja kuzisoma Buhuthi(tafiti za kielimi)zao juu ya historia sahihi ya Sheikh Muhammad bin Abdil wahabi,   na maisha yake ya kidaawa,na tuhuma anazopewa na maadui zake,tafiti ambazo walizifanya pindi walipo takiwa kufanya hivyo.

Baada ya kusomwa Buhuthi hizo,ziliandikwa kitabu chenye juzuu mbili kitwacho
"Buhuthu nad'wati da'awatis Sheikhi Muhammad bin Abdil wahabi"

chapa niliyo nayo mimi ni ya mwaka 1411 h,sawa na1991ad, baada ya siku hiyo haikufanyika tena semina hiyo hadi leo sambe hiyo- inayoitwa na wazushi kuwa ni-sherehe.

Saudia haiko mbinguni,wala umbali wa kutoweza kufika watu,hebu waulizeni watu walioko huko je,mlishawahi kusikia kwamba huko Saudia kuna wiki ya kumsherehekea Muhammad bin Abdil wahabi?au sherehe ya yoyote yule katika maulamaa au viongozi?

2-Saudia ni kama nchi nyingine duniani-pamoja na kwamba ndiyo nchi pekee duniani inayo simamisha sheria ya kiislamu,pamoja na mapungufu yaliyo kuwepo-lakini siyo hoja katika uislamu,ya kuambiwa watu kwamba; mbona Saudia wafanya kadha,sisi hatuangalii Saudia wala nchi yoyote,tunachoangalia sisi ni maandiko ya kisheria,na kauli za Ulamaa wakubwa zilizo jengwa juu ya hoja na dalili za kisheria.

3-Hebu tunapo kuwa tunatoa hukumu ya mambo tuwe waadilifu,chuki binafsi zisituzuwie kufanya uadilifu,mpaka kufikia kuwazulia watu mambo ambayo hawakuyafanya ili tu muradi wetu utimie,amesema mwenyezi mungu{s.w.t.};

*"...wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutowafanyia uadilifu.fanyeni uadilifu huko ndiko kunakomkurubisha mtu na ucha Mungu*.."
surat maida(4) aya ya (8).

## Hoja yao ya saba;

Bwana Mtume{s.a.w.}ni reh'ma na ni fadh'la kubwa kabisa itokayo kwa mwenyezi mungu,na mwenyezi mungu ametuamrisha katika Qur'an tuisherehekee reh'ma na fadh'la hii pale aliposema;

قُلْ بِفَضْلِ اللّهِ وَبِرَحْمَتِهِ فَبِذَلِكَ فَلْيَفْرَحُواْ هُوَ خَيْرٌ مِّمَّا يَجْمَعُونَ {يونس58
[sema kwasababu ya fadhila za mwenyezi mungu,na reh'ma zake,kwasababu ya hilo basi na wafurahi,hilo ni bora kuliko vile wanavyo vikusanya].

Sasa basi kuna ubaya gani sisi kukusanyika na kusherehekea?

## Jawabu ni kama ifuatavyo;

Ni kweli kwamba Bwana Mtume{s.a.w.} ni Reh'ma kubwa itokayo kwa mwenyezi mungu,na hili bila shaka hakuna muislamu anaye lipinga,na nikweli kabisa kwamba aya imekuja kutuamrisha tuisherehekee reh'ma hii,

kwahivyo ni wazi kwamba kumsherehekea/kumfurahikia Bwana Mtume{s.a.w.} ni ibada,na kama ni ibada,je ninani anayepanga taratibu za ibada?

Ni yeye Bwana Mtume{s.a.w.} au kila mtu yuko huru kujifanyia atakavyo?

Bila shaka kwamba katika masuala ya ibada hakuna uhuru wa mtu kujifanyia atakavyo, nisharti kufuata utaratibu wa kisheria,na hili hakuna muislamu mwenye akili timamu anaye weza kulipinga seuze huyo anayeitwa kuwa ni msomi.

Kama ndivyo hivyo basi,je huo utaratibu wa kisheria alio ufundisha Mtume{s.a.w.} ndiyo hii mikusanyiko ya maulidi?

bila shaka Mtume{s.a.w.} hakufundisha maulidi,na ameondoka duniani dini imekamilika,na ujumbe umekamilika na maulidi hayamo.

Na kama hakufundisha maulidi nyinyi mmeyatoa wapi?hebu tuelezwe huyo aliyewafundisha uzushi huu ninani? wapi? lini? kwanini? na je huyo aliye wawekea haya maulidi anajua zaidi utaratibu wa dini kumshinda Mtume{s.a.w.} na maswahaba zake?

-na hivyo mlivyo ifahamu nyinyi hiyo aya kwamba maana yake ni kukusanyika kusoma maulidi,ninani katika maswahaba au walio waandimia,au maimamu wakubwa aliyefahamu hivyo?na kwanini wao hawakusoma maulidi?hii inaonyesha wazi kwamba aya hii mmeifahamu kimakosa.

Na kama ufahamu wenu ni sahihi hebu tutajieni mfasiri mmoja tu miongoni mwa wafasiri wa kubwa wenye kutegemewa aliyeitafsiri aya hii kwamba maana ya aya hii hapa ni kusoma maulidi, kama hakuna,basi mjuwe wazi kwamba nyinyi ni wazushi,na mnafuata matamanio ya nafsi zenu,na hayo ni katika mambo yanayo wazuia kuifikia haki.

## Hoja yao ya nane;

Je ni jambo gani  ambalo sisi tunalifanya katika maulidi lakini halimo katika dini?

Sisi tunapo soma maulidi tunafanya haya;

-Tunaanza maulidi kwa kusoma Qur’an.

-Halafu tunasoma dua(tawassuli) nasisi tumeamrishwa   kuomba mungu.

-Tunasoma utenzi kumswalia Mtume{s.a.w.}.

-Halafu tunaimba kasida za kumsifu mtume{s.a.w.} na maswahaba walikuwa wakimsifu mtume{s.a.w.}kwa mashairi mbele yake.

-Kisha tunapeana mawaidha,na sisi tume amrishwa kuamrishana mema na kukatazana maovu.

-Kisha tunalishana chakula,na hilo pia tumearishwa na uislamu.
-na faida ya mikusanyiko hii,waislamu wanatembeleana, wanajuana, wanapendana,bali kuna watu wengi wanasilimu kupitia haya maulidi.
sasa ndugu zetu mpingao maulidi, katika haya tuliyo yataja baya nilipi lisilo la kiislamu? hebu tuelezwe!

kwa ufupi ni kwamba,kwani maulidi yana ubaya gani??
hii pia ni miongoni mwa hoja ya kiakili ambayo ni ya mtaani,lakini masheikhe zao pia wanaitumia.

**Jawabu yake ni kwa njia tatu;**

1-hoja hii nyonge inajibiwa na swali hili;
hivi unajua ni kwanini Ibin Masoud aliwakataza wale walio kusanyika msikitini wakifanya dhikri?

kwani lile walilokuwa wakilifanya lina ubaya gani?

Jawabu ya swali hili ndiyo jawabu ya hoja hiyo.

Pengine anaweza kujitokeza mtu ambaye ni mgonjwa wa moyo na akili akasema bila ya kujali;

Yale aliyo yasema Ibin Mas'oud ni kwa ij'tihadi yake binafsi kwahiyo si hoja!

Sisi tunasema kwamba hizo ni fik'ra nyonge za kishia za kuwachukia maswahaba wa Mtume{s.a.w.},ama kwa mtazamo sahihi wa kiislamu ni kwamba kauli ya swahaba ni hoja muda wa kuwa haipingani na kauli ya swahaba mwengine,
na hakuna kauli ya swahaba mwengine iliyo kinyume na kauli hii,kama ipo hebu na itajwe,ni swahaba gani?alipo semaje?

2-Na bila shaka utaratibu huo mseto hakuufundisha Mtume{s.a.w.} wala maswahaba,pamoja na kuwa sababu zilikuweko,na hakukua na vizuizi vyovyote.

Na Mtume{s.a.w.} anatwambia kwamba;

من أحدث فى أمرنا هذا ما ليس منه فهو رد.

[Mwenyekuzusha katika dini yetu hii jambo lisilokuwemo,basi jambo hilo ni lenye kurudishwa].Halitokubaliwa.

na amesema Imamu Malik{r.a.};

فما لم يكن يومئذ دينا فلا يكن اليوم دينا...

[…Basi lile ambalo halikuwa dini siku hizo, haliwezi likawa ni dini hii leo..]

Na tunakubaliana sote kwamba utaratibu huu mseto umezushwa katika dini baada ya kar'ne tatu bora,kwa hivyo haukubaliki,bila ya kuangalia eti kuna watu wanasilimu au la, kama kusilimu watu ndiyo hoja ya kufaa kwa uzushi huu,basi hata madogori(ngoma za kupungwa shetani) yanafaa maana watu pia husilimu kwenye kupungwa na kukabidhiwa mikoba!!

Na hata hayo madogori pia hufunguliwa kwa kusomwa Qur'an!! Je nayo yafaa?!

3-Pamoja na uzushi wote huo,kumezalikana katika mikusanyiko hiyo mambo mengi maovu ambayo hayakubaliki kisheria.

Kwa hiyo mikusanyiko ya maulidi ni moja kati ya njia zinazo changia kupatikana maovu hayo,kwa hiyo ni lazima ifungwe njia hiyo, huwenda baadhi ya watu walio na ufahamu duni wa dini wakasema;

"Kwanini maulidi yote yatupwe kwasababu tu yakufanywa baadhi ya mambo ambayo ni munkar katika sherehe zake? Kwanini hayaondolewi hayo ya munkar,kama yako,yakabakishwa yasiyo ya munkar?

Kwani tunda likiwa limeoza kidogo hutupwa lote,au hukatwa pale palipooza likaliwa pazuri palipobaki?

Jawabu ni kwamba,tunda hili ni miongoni mwa yale matunda yasiyoliwa,kisha kwa bahati mbaya tunda lenyewe limeoza! hivyo halifai as'lan,na hapo palipooza pamezidisha kutokufaa kwake,kwa hiyo hata ulikate palipooza bado litabaki halifai!!

Na ama hoja ya kusema kwamba,kwani maulidi yana ubaya gani?hii ni miongoni mwa hoja zilizoiharibu dini yakina Paulo,na walillahil hamdu wakina paulo hawana nafasi katika dini hii,kama uzushi huu wa maulidi hauna ubaya wowote basi hata kheri hauna,na kama una kheri basi kwanini hakuifundisha Bwana Mtume{s.a.w.} mpaka wakaja watu wenye asili ya kiyahudi na kimajusi ndiyo wakayaanzisha?!kwa hoja eti wanasherehekea mazazi ya mtume{s.a.w.}!!

Na hatulipingi hili eti kwasababu tu limeanzishwa na mayahudi,bali ni kwa hoja na dalili nyingi ambazo zinapinga na kutahadharisha kuzusha mambo ambayo hayakufundishwa katika dini,miongoni mwa hayo ambayo hayakufundishwa katika dini ni hii mikusanyiko ya maulidi.

Na kwasababu jambo hili ni ibada basi ni lazima zipatikane hoja na dalili za kulithibitisha jambo hili,na kama kuna yoyote yule anaedai kwamba Bwana Mtume {s.a.w.} amewafundisha maswahaba zake kukusanyika kwa ajili ya mazazi yake anatakiwa alithibitishe hilo kwa hoja na dalili za kisheria,na siyo kwa hoja za kina paulo,eti kuna ubaya gani?!

**الأصل فى العبادات التوقف الا بالنص**

Kwasababu; "Asili katika mambo ya ibada ni kusimama(kusubiri) mpaka lije andiko" (la kuidhinisha).

Na hakuna andiko lililowaidhinisha kukusanyika kwa ajili ya kuadhimisha mazazi ya Bwana Mtume{s.a.w.} ndiyo maana mkakimbilia kusema kwamba hiyo mikusanyiko yenu si ibada-kama tulivyotaja katika hoja yenu ya nane-ili kukikwepa kipengele hiki.

Kwasababu mnajua kwamba mkisema kwamba hiyo mikusanyiko yenu ni ibada mtahitajika kuleta dalili ya kisheria kulithibitisha hilo,kwahiyo itawawilia vigumu kufanya hivyo kwasababu hamna dalili,kwahiyo mkaona mseme kwamba maulidi si ibada,nayo ndiyo hii..

## Hoja yao ya tisa;

Wanasema hivi;

"Sisi hatusemi kwamba maulidi ni ibada! bali tunasema kwamba maulidi ni ada tu miongoni mwa ada zilizo nzuri, na mambo ya ada asili yake kisheria ni uhalali,mpaka itakapokuja dalili ya kuharamisha,na hakuna dalili yoyote ya kuharamisha kusoma maulidi,na mwenye kuyasoma maulidi hatakiwi alete dalili,bali dalili anatakiwa alete mwenye kupinga,
na mpaka leo hii hatuja pewa dalili hata moja inayosema maulidi ni haramu! na kama ipo basi tupewe dalili hiyo,
Kwahivyo basi,siyo insafu kwa ndugu zetu wanaopinga maulidi kung'ang'ania kututaka sisi tutoe hoja na dalili za kufaa kwa maulidi,na hali ya kuwa kisheria wao ndio wanao takikana watoe hoja za kuharamisha".

**Jawabu ni kama ifuatavyo;**

1)kudai kwamba maulidi si ibada,bali ni katika ada zilizo nzuri,ni moja katika njia za kuukimbia ukweli kwasababu zifuatazo;

a)kabla hawajajitokeza wapingaji wa maulidi katika miji yetu ya Afrika ya mashariki,na kupata nguvu, masheikh na waalimu walikuwa wakiwaambia wafuasi wao wajitolee kwa hali na mali ili kuyafanikisha maulidi na wakifanya hivyo watapata ujira mbele ya Allah{s.w.t.}!

Na huku wakisomewa aya na hadithi tele zinazo ishiria fadhila za kujitolea katika jambo hili la maulidi,na kuwaambia kwamba ukihudhuria maulidini kila hatua unapata thawabu!

Na hiyo ni ishara ya wazi ya kwamba jambo hilo walikuwa wanaitakidi kwamba ni dini,basi vipi mnawaahidi watu kupata thawabu kwa kila hatua wanayopiga kuhudhuria katika jambo ambalo halihusiani na dini kwa njewe wala sikio?! Au hizo thawabu nyie ndio mnao zigawa?

Sasa je,hii leo mnataka kuwaambia hao mlio kuwa mkiwahamasisha,kwamba yale tuliyokuwa tukiwaambia ni maneno ya urongo?
Na ukweli ni huu wasasa baada ya kujitokeza wapingaji?

Kwahiyo mmepoteza nguvu zenu na mali zenu bure bila ya kupata thawabu wala ujira?!

b)Wanawatuhumu wanaopinga maulidi kwamba hawampendi mtume{s.a.w.} kwasababu tu kwamba hawakubaliani na jambo hilo,na mtu kama hampendi Mtume{s.a.w.} si muislamu,sasa basi vipi mnawatowa watu katika uislamu kwasababu ya kulipinga jambo ambalo si ibada bali ni ada tu?!

2)Bila shaka ndugu zetu wanaosoma maulidi wanapofanya maulidi yao wanataraji kwamba wanapata thawabu kwa kufanya jambo hilo,na bila shaka kwamba jambo hili wameliwekea utaratibu maaalumu,na ilivyothibiti katika misingi ya kielimu ni kwamba jambo lolote ambalo ni ada likiwekwa katika mtindo wa kiibada basi jambo hilo linakuwa lina hukumu ya ibada na litahitaji dalili ya kulihalalisha.

Amesema Imamu Shatwiby;

فالحاصل أن أكثر الحوادث التى أخبر بها النبي صلى الله عليه وسلم من أنها تقع وتظهر وتنتشر
...لامن جهة كونها عادية,لكن من جهة التعبد, أمور مبتدعة على مضاهاة التشريع
ان العاديات من حيث هي عادية لا بدعة فيها
. ...ومن حيث يتعبد بها أو توضع موضع التعبد تدخلها البدعة ,

[Na natija iliyopatikana ni kwamba matukio mengi aliyo yaeleza Mtume{s.a.w.} kwamba yatapatikana na kudhihiri na kuenea katika mambo ya bidaa ni kwa kule kufanana kwake na mambo ya kisheria,lakini (hilo) katika ule upande wa kiibada,na siyo kwa upande wake wa kiada… Kwasababu mambo yote ya ada muda wa kuwa yako katika ada hayana bidaa,lakini ya kisha fanywa ni ibada,au yakiwekwa mahala pa ibada basi yanaingiwa na bidaa…]
tazama kitabu Al i'tiswaam 2/385.

Na hili jambo la maulidi limewekwa mahali pa ibada,kwa kuwa hayo yanayofanyika ndani ya mikusanyiko ya maulidi ni mambo ya kiibada ambayo nyinyi mmeyawekea utaratibu na mfumo usio kuwa wa kisheria, tena bila ya idhini ya sheria,kisha wafanyaji wa hayo wanataraji kupata thawabu kwa kufanya amali yao hiyo! Sasa vipi leo hii mnadai kwamba maulidi siyo ibada,bali ni ada tu?! Ama kweli mtu akipenda chongo huiita kengeza!

Au mnataka kutuambia kwamba siku hizi mkikusanyika katika maulidi,mnakusanyika kwa ajili ya kuvua samaki na kuwinda paa?au mnakusanyika kwa ajili ya kumswalia Mtume {s.a.w.} kwa mitindo mliyoibuni?

Je kumswalia Mtume {s.a.w.} nako siku hizi si ibada tena ni ada tu? au hiyo hoja yenu ya saba hamuitaki tena?au mmeisahau? na hilo pia si

ajabu,kwasababu hoja zenu nyinyi ni za kubuni ndiyo maana (zina tanaaqudhi) zinajigonga sana,na hii ndiyo natija ya kuikimbia haki.

Enyi ndugu zangu nyie! Hebu rudini katika haki,kwani kujirudi na kuifuata haki ni fadh'la na si unyonge.

## KHATIMA;

Mwisho wa makala hii tunahitimisha kwa kutaja vipengele muhimu vya sheria,ili vikusaidie ndugu yangu muislamu kupambana na bidaa na watetezi wake popote pale ulipo,ili uweze kuwatibu ndugu zetu ambao wameathiriwa na gonjwa hili hatari la uzushi katika dini,gonjwa ambalo limesababisha kudhoofika umma wa kiislamu kwasababu ya kuleta far'ka na mpasuko katika safu zao,na ndipo maadui wakaitumia fur'sa hii kuwatweza na kuwadhalilisha waislamu.

*Muongozo wetu katika dini ni Qur'an na Sunna za mtume{s.a.w.} kama walivyo fahamu maswahaba{r.a.} na waliowafuatia wao kwa wema.

*Jua ndugu yangu muislamu kwamba jambo lolote la dini ambalo hakulifanya Bwana Mtume{s.a.w.} wala hakulifundisha, pamoja na kwamba kulikuweko na sababu ya kulifanya jambo hilo,na wala hakukuweko na kizuizi chochote kilicho mzuia.

Kulifanya jambo hilo baada ya kuondoka yeye{s.a.w.}ni kuzusha katika dini jambo lisilo kuwemo,na kufanya hivyo ni upotevu unaopelekea kuingia motoni,amesema Mtume{s.a.w.};

[..Tahadharini na mambo ya uzushi-katika dini- kwani kila lenye kuzuliwa-katika dini- ni bidaa,na kila bidaa ni upotevu,na kila upotevu ni motoni].

Mfano wa jambo hilo ni kama kuweka adhana kwa ajili ya swala za eid,na kuzusha mikusanyiko ya maulidi.

*Kuyawekea mifumo/utaratibu mambo ya dini tofauti na utaratibu wa kisheria ni kuzusha katika dini yasiyo kuwemo,amesema Mtume{s.a.w.};

[Mwenye kuzusha katika dini yetu hii jambo lisilo kuwemo basi jambo hilo ni lenye kurudishwa].
Halitokubaliwa.kama kuweka utaratibu/mfumo maalumu wa kumdhikiri Allah {s.w.},au utaratibu/mfumo maalumu wa kumswalia mtume{s.a.w.} na kumsherehekea bwana huyu..

*Jambo lolote lile la dini ambalo maswahaba{r.a.} wamelifanya baada ya kuondoka bwana mtume{s.a.w.} kwa kupatikana sababu au kwa kuondoka vizuizi vilivyomzuia mtume{s.a.w.} katika uhai wake,kulifanya jambo hilo si bidaa,bali ni sunna,kama kuiandika Qur'an katika msahafu mmoja,kuindeleza swala ya tarawehe kwa jamaa,kuwapigavita walio ritadi na kuzuia zaka.

*Bidaa zote katika dini ni mbaya na ni upotevu,na hakuna bidaa nzuri,na bidaa haiingii katika mambo ambayo si ibada kama vile kupanda ndege,gari,baiskeli,na n.k. amesema mtume{s.a.w.};[Nyinyi mnajua zaidi mambo ya dunia yenu].

Hivyo basi siyo sahihi kwa wazushi katika dini wanapokatazwa kuzusha katika dini haraka wao wakaanza kujitetea ooh! Kama kila kilichozushwa ni bidaa,na kila bidaa ni upotevu,basi magari ni bidaa pikipiki bidaa,feni bidaa,busati bidaa,ac bidaa,computer bidaa!

hii inaonyesha wazi kwamba ima hawaijui ni nini maana sahihi ya bid'a kisheria, au wanaijua lakini lengo lao ni kutaka kuwapoteza watu,au wanasifa zote mbili.

*Mwisho tunasema kwamba mikusanyiko ya maulidi ni haramu tena ni uzushi mbaya katika dini,na uzushi ni ugonjwa mbaya ulioleta far'ka katika

umma wa kiislamu hivyo basi.haifai kwa waislamu kuyafanya mambo hayo baada ya kujua.

Ama wazee wetu na masheikh zetu waliotangulia mbele za haki mwenyezi mungu -Inshaallah- atawasamehe sababu ni kwamba ukweli ulikuwa haujawadhihirikia, ama wewe uliye dhihirikiwa na haki kisha ukaipiga teke,ujuwe kwamba huna hoja ya kujieleza mbele ya Allah {s.w.t.},na ninakuhusia usijipe sifa za washirikina wa Makka,wao walikuwa wakijiliwa na jambo la haki hulipiga teke na huku wanasema hivi;

[Hakika sisi tumewakuta wazee wetu juu ya mila hii na sisi ni wenye kufuata athari zao.].

Huu ndio mwisho wa makala kuhusu
ATHARI MBAYA YA UZUSHI KATIKA UISLAMU.

Bila shaka ndugu yangu umepata faida kwa kusoma makala hii,kwahiyo tunaomba dua zako za kheri kwa muandishi na wote waliosaidia kuitawanya makala hii,mpaka ikakufukia,bila kusahau kuwaombea waislamu wote.
na ufahamu kwamba ukamilifu ni wa Allah {s.w.t.} peke yake,hakuna mwana adamu asiye kosea ila wale waliolindwa na Allah s.w.t.

**Tafadhali fuatilia mfululizo wa makala zetu;**

**1,2,3,)Athari mbaya ya uzushi katika uislamu.**

**(namba tatu ndiyo hii iliyo mikononi mwako).**

**4,5,6,)Uharamu wa kuyajengea makaburi.**

**وصلى الله وسلم وبارك على سيدنا محمد وعلى آله وصحبه أجمعين,**
**والحمد لله رب العا لمين.**